JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

# BODI YA KOROSHO TANZANIA



# JARIDA LA MWEZI JULAI 2023.

**Toleo Jipya**

**#KilimoBiashara**

## 1.0 UTANGULIZI

Soko la zao la korosho duniani bado halijatengamaa vizuri, hii imesababishwa na kushuka kwa mahitaji ya korosho karanga katika nchi za bara la Ulaya, Asia na Amerika ambako kuna walaji wakubwa wa korosho. Ingawa jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanyika ili kunusuru hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza ubanguaji wa korosho na kuzalisha bidhaa zingine zitokanazo na korosho.

Ingawa kumekuwa na changamoto ya kupanda na kushuka kwa bei ya korosho, uzalishaji wa korosho ghafi umekuwa ukiongezeka duniani na kuongeza ushindani kwa nchi wazalishaji, huku India na Vietnam wakiwa ndio wanunuzi wakubwa wa korosho ghafi zinazozalishwa duniani kote.



## 2.0. MWENENDO WA SOKO LA KOROSHO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI MWEZI JULAI, 2023.

### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Nchini Ivory Coast msimu wa mauzo ya korosho ghafi umefika mwisho, kutokana na kuendelea kwa upatikanaji wa korosho ghafi kutoka shamba, baadhi ya viwanda vya ndani vinatumia nafasi hiyo kuongeza malighafi kwenye hifadhi zao.

Bei bado ni ndogo na ubora bado ni duni, bei hutofautiana kati ya Dola za Kimarekani **0.25** hadi **0.42 (TZS 612.39 hadi 1,028.82)** kwa kilo moja katika soko la ndani.

Nchini Ghana msimu wa mauzo umeisha, Kutokana na takwimu za kibiashara kuanzia Januari hadi Mei **2023,** Ghana iliuza korosho ghafi nje tani 258,762 huku India ikinunua kiasi kikubwa cha korosho jumla ya tani 167,658 sawa na 65% na ikifuatiwa na Vietnam tani 82,041 sawa na 32%

.

Nchini Benin pia msimu wa mauzo ya korosho unaelekea mwisho na shughuli za usafirishaji bado zinaendelea. Kunaripotiwa kuendelea kuwepo kwa mauzo katika baadhi ya vituo ingawa sio kwa kiwango kikubwa. Maoni kutoka kwa wanunuzi wanadai kuwa ubora bado ni wa kiwango kizuri. Kumekuwa na ongezeko kidogo la bei katika mji wa Cotonou ambayo ni Dola za Kimarekani **0.56 (TZS 1,371.76)** kwa kilo moja.

Bei katika maeneo mengi ya uzalishaji ni takribani Dola za Kimarekani **0.49** hadi **0.50 (TZS 1,200.29 hadi 1,224.79)** kwa kilo moja katika soko la ndani kutokana na ubora wa korosho ghafi.



**Ivory Coast**



**Ghana**



**Benin**



**Uganda**



**India**

**Nchini Burkina Faso** msimu wa mauzo umeisha, hata hivyo bado kuna kiasi cha korosho kipo kwa wakulima lakini ubora ni duni kwa sababu ya mvua na uhifadhi wa korosho katika maeneo yasiyo sahihi. Bei katika ngazi ya mkulima ni karibu Dola za Kimarekani **0.40** hadi **0.42 (TZS 979.83 hadi 1,028.82)** kwa kilo moja.

**Nchini Nigeria** ingawa msimu rasmi wa mauzo umeisha ila kuna kupanda kidogo kwa bei ya korosho ghafi katika masoko mbalimbali. Hii ni kwa sababu nchi nyingi zimefunga msimu na hazina korosho za kutosha. Soko la Nigeria bado lina ubora unaoridhisha wa korosho ghafi ambapo kwa miji ya Ogbomoso na Ilorin ubora unaanzia kwa **Ratili 44** hadi **46 (44-46lbs)** na mji wa Lagos ubora ni Ratili 47 (47lbs), bei ni takribani Dola za Kimarekani 0.39 hadi 0.52 (TZS 955.34 hadi 1,273.78) kwa kilo moja



## 2.2. HALI YA SOKO LA KOROSHO NCHINI INDIA

Nchini India mahitaji ya soko la ndani la korosho karanga yameendelea kupanda katika mwezi Julai baada ya kupitia kipindi kigumu mahitaji yanaongezeka kwa madaraja mengi ya korosho karanga. Bei zimeongezeka kwa Dola za Kimarekani 0.18 hadi 0.24 kwa kilogramu kwa madaraja mbalimbali (ambayo yanaweza kutofautiana kutoka soko moja hadi jingine). Korosho ghafi iliyoagizwa kutoka Benin imenunuliwa kwa takribani Dola za Kimarekani 1,100 kwa tani kwa korosho zenye ubora wa ratili 48 (48lbs)

## 2.3. HALI YA SOKO LA KOROSHO KATIKA NCHI YA VIETNAM

Nchini Vietnam soko la korosho ghafi limebaki imara kwa mwezi Julai, ambapo kiasi kikubwa cha korosho zenye ubora wa daraja la juu kutoka Afrika kimenunuliwa ingawa kuna kiwango kidogo kimenunuliwa cha korosho zenye ubora wa daraja la chini. Soko la korosho karanga bado halijawa thabiti, ofa zimekuwa ni chache mno kutoka kwa wanunuzi pia bei imekuwa ni ya chini na kusababisha wauzaji kukataa kuuza kwa kuhofia kupata hasara. Baadhi ya wauzaji wako kwenye shinikizo la kulipia korosho ghafi zilizowasili bandarini kutoka Afrika hivyo wanauza korosho karanga kwa bei ya chini ili wapate pesa za kulipia shehena iliyopo bandarini kwa mujibu wa mikataba waliyoandikishana.



**JEDWALI NA.1:**
**BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA NCHI YA INDIA NA VIETNAM JULAI, 2023**

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI DUNIANI INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA NOVEMBER 2022 HADI JULY, 2023 | | |
|---|---|---|
| TARAHE | Bei - CIF USD / TON | |
| | | BEI YA JUU |
| 27 Novemba,2022 | 1,100 | 1,4000 |
| 12 December, 2022 | 1,100 | 1,330 |
| 24 Desemba, 2022 | 1,150 | 1,320 |
| 24 Desemba, 2022 | 1,150 | 1,320 |
| 14 Januari, 2023 | 1,200 | 1,275 |
| 28 Januari, 2023 | 1,250 | 1,39 |
| 18 Februari, 2023 | 1,180 | 1,230 |
| 13 Machi, 2023 | 1,150 | 1,165 |
| 24 Aprili, 2023 | 1,040 | 1,080 |
| 20 Mei, 2023 | 1,040 | 1,130 |
| 18 Juni, 2023 | 925 | 1,065 |
| 22 Julai, 2023 | 925 | 1,080 |
| SOT: 46-51 | | |

**Chanzo:** Cashewnutinformatio

## 3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji, viwango vya ubora pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

### 3.1 BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM KUFIKIA JULAI, 2023

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ikilinganishwa na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko madogo ya bei kwa mwezi Julai kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2

**JEDWALI NA. 2: BEI ZA KOROSHO KARANGA NCHINI VIETNAM HADI KUFIKIA JULAI, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA JULAI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAUZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Juu | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | 180 WW | 7.72 | 7.94 | 18,396.76 | 1 8,921.02 |
| White Whole Cashews 210 | WW 210 | 6.62 | 6.84 | 15,775.46 | 16,299.72 |
| White Whole Cashews 240 | WW240 | 5.62 | 6.00 | 13,392.46 | 14,298.00 |
| White Whole Cashews 320 | WW320 | 5.47 | 5.62 | 13,035.01 | 13,392.46 |
| Large Pieces | LP | 3.09 | 3.53 | 7,363.47 | 8,411.99 |
| Small Pieces | SP | 2.43 | 2.65 | 5,790.69 | 6,314.95 |

**Chanzo:** Cashewinformation

### 3.2 BEI YA KOROSHO KARANGA KATIKA NCHI ZA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA JULAI, 2023

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Julai, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni pamoja na Ivory Coast, Ghana na Benin ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

**JEDWALI NA. 3: BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA JULAI, 2023**

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA JULAI, 202 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) | | Bei TZS/Kilo (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180 | 180 | | | | |
| White Whole Cashews 180 | W 210 | 7.17 | 7.72 | 17,086.11 | 18,396.76 |
| White Whole Cashews 240 | W240 | 5.73 | 6.13 | 13,654.59 | 14,607.79 |
| White Whole Cashews 320 | W320 | 5.51 | 5.73 | 13,130.33 | 13,654.59 |
| White Whole Cashews 450 | W450 | 5.18 | 5.40 | 12,343.94 | 12,868.20 |
| White Splits | WS | 3.86 | 4.19 | 9,198.38 | 9,984.77 |
| Large Pieces | LP | 3.20 | 3.53 | 7,625.60 | 8,411.99 |
| Small Pieces | SP | 2.54 | 2.76 | 6,052.82 | 6,577.08 |

**Chanzo:** Cashewinformation

## 3.3 BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE YA NCHI HADI KUFIKIA JULAI,2023.


Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni, Marekani nk. Ni kama ilivyo katika jedwali Na. 4

### JEDWALI NA. 4: BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE YA NCHI HADI KUFIKIA JULAI, 2023.

| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA JULAI, 2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO YA DARAJA | DARAJA | BEI DOLA/KILO (FOB) | | BEI TZS/KILO (FOB) | |
| | | Bei ya Chini | Bei ya Juu | Bei ya Chini | Bei ya Juu |
| WHITE WHOLE CASHEWS 180 | W180 | 7.58 | 8.15 | 18,063.14 | 19,421.45 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 240 | W240 | 6.91 | 7.19 | 16,466.53 | 17,133.77 |
| WHITE WHOLE CASHEWS 320 | W320 | 6.33 | 6.62 | 15,084.39 | 15,775.46 |
| WHITE SPLITS | WS | 4.50 | 4.50 | 10,723.50 | 10,723.50 |
| LARGE WHITE PIECES | WS | 4.50 | 4.50 | 10,723.50 | 10,723.50 |

**Chanzo:** Tanzania Association for Cashewnut Processors **(TACP)**

**JEDWALI NAMBA 5: UWIANO WA BEI DARAJA WW320**




**Chanzo:** Bodi ya Korosho

## 4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA.

Hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2023 uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2022/2023 ni tani 189,113.799 zenye thamani ya shilingi 347,776,155,945.00 ambapo tani 176,749.451 zimekusanywa na kuuzwa katika ghala za minada zenye thamani ya shilingi 328,362,003,965.00. Mauzo ya korosho kupitia soko la awali hadi kufikia wiki ya mwisho ya mwezi Julai ni tani 4,683.770 zenye thamani ya shilingi 7,893,284,650.00 na korosho zilizobanguliwa na wabanguaji wadogo ni takribani tani 1,706.795 sawa na tani 7,680.578 za korosho ghafi zenye makadirio ya thamani ya shilingi 11,520,867,330.00. Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji unaendelea.

Shughuli ya utoaji wa vibali vya kusafirisha Korosho ghafi nje ya nchi inaendelea ambapo hadi sasa zaidi ya tani 169,111.648 za korosho ghafi zenye thamani ya Dola za Kimarekani 155,991,960.88 (FOB Value) zimepatiwa vibali vya kusafirisha nje ya nchi. Pia vibali vya kusafirisha korosho karanga vinaendelea kutolewa na hadi sasa zaidi ya tani 1,301.888 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 6,770,950.22 (FOB Value) zimesafirishwa.



# MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI.

## JEDWALI NA. 6A: TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 HADI KUFIKIA MWEZI JULAI, 2023

## TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 HADI KUFIKIA TAREHE 31/07/2023

| | MKOA | CHAMA KIKUU | GHALA ZA MNADA (KG) | THAMANI GHALA ZA MNADA (TSHS) | SOKO LA AWALI (KG) | THAMANI SOKO LA AWALI (TSHS) | ZILIZO BANGULIWA (KG) | | THAMANI UWIANO WA GHAFI (TSHS) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | ZILIZO BANGULIWA | UWIANO WA GHAFI | |
| 1 | MTWARA | TANECU | 33,518,494.00 | 63,447,865,104.00 | 1,486,294.00 | 2,411,476,400.00 | 1,101,325.50 | 4,955,964.75 | 7,433,947,125.00 |
| | | MAMCU | 33,518,494.00 | 63,447,865,104.00 | 1,486,294.00 | 2,411,476,400.00 | 1,101,325.50 | 4,955,964.75 | 7,433,947,125.00 |
| 2 | LINDI | RUNALI | 42,440,859.00 | 81,187,464,564.00 | 7,200.00 | 11,520,000.00 | 2,611.00 | 11,749.50 1 | 7,624,250.00 |
| | | MWAMBAO | 14,622,801.00 | 25,590,331,828.00 | 654,964.00 | 1,132,707,300.00 | 210,413.86 | 946,862.37 | 1,420,293,555.00 |
| 3 | RUVUMA | TAMCU | 15,156,209.00 | 26,809,585,960.00 | 126,446.00 | 191,965,000.0 | | | |
| 4 | PWANI | CORECU | 10,759,505.00 | 18,796,294,846.00 | 1,415,619.00 | 2,468,173,500.00 | 269,043.00 | 1,210,693.50 | 1,816,040,250.0 |
| 5 | TANGA | TACACU | 378,873.00 | 625,219,005.00 | | | 6,520.80 | 29,343.60 | 44,015,400.0 |
| 6 | SINGIDA | CEAMCU | 23,208.00 | 41,890,440.00 | 18,769.00 | 30,968,850.00 | | | |
| 7 | MOROGORO | MOFACU | 153,959.00 | 264,846,120.00 | - | - | - | - | - |
| 8 | TABORA | | | | 2,000.00 | 3,000,000.00 | - | - | - |
| 9 | DODOMA | DOMASIKA | 24,079.00 | 40,164,540.00 | - | - | | | |
| 10 | MBEYA | TAMCU | 25,850.00 | 45,418,450.00 | 404.00 | 666,600.00 | | | |
| 11 | NJOMBE | TAMCU | 35,947.00 | 63,158,879.00 | | | | | |
| 12 | KIGOMA | | | 10,000.00 | 15,000,000.00 | | | | |
| | JUMLA NDOGO | | 176,749,451.00 | 328,362,003,965.00 | 4,683,770.00 | 7,893,284,650.00 | 1,706,795.16 | 7,680,578.22 | 11,520,867,330.00 |
| | JUMLA KUU UZALISHAHI | | | | | | | | 189,113,799.22 |
| JUMLA KUU DHAMANI | | | | | | | | | 347,776,155,945.00 |

**NB:** Taarifa hii ya uzalishaji ni hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2023.
Ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji bado unaendelea.

## JEDWALI NA. 6B: USAFIRISHWAJI WA KOROSHO KARANGA TANZANIA KWENDA NCHI MBALIMBALI KUANZIA SEPTEMBA 2022 HADI JULAI, 2023.


| NO | NCHI | BKIASI | THAMANI (FOB VALUE) |
|---|---|---|---|
| 1 | **Angola** | 2,100.00 | 6,000.00 |
| 2 | **Austria** | 20,838.00 | 132,592.53 |
| 3 | **Ubelgiji** | 16,529.00 | 79,411.96 |
| 4 | **Canada** | 19,005.00 | 72,400.00 |
| 5 | **China** | 93,249.80 | 420,088.45 |
| 6 | **Misri** | 210,064.00 | 780,330.00 |
| 7 | **Ujerumani** | 14,167.00 | 97,470.00 |
| 8 | **Iraq** | 62,276.64 | 273,757.35 |
| 9 | **Kenya** | 20,169.00 | 103,845.00 |
| 10 | **Kuwait** | 104,045.46 | 487,797.06 |
| 11 | **Lebanon** | 10,500.00 | 40,000.00 |
| 12 | **Morocco** | 16,584.00 | 93,568.10 |
| 13 | **Uholanzi** | 249,111.04 | 1,603,034.12 |
| 14 | **Oman** | 14,700.00 | 65,800.00 |
| 15 | **Saudi Arabia** | 15,225.00 | 61,625.00 |
| 16 | **Slovenia** | 148,945.40 | 981,935.50 |
| 17 | **Afrika Kusini** | 21,874.24 | 117,666.72 |
| 18 | **Uturuki** | 78,645.90 | 410,792.94 |
| 19 | **Uganda** | 30,035.00 | 147,326.70 |
| 20 | **Umoja wa Falme za Kiarabu** | 51,999.00 | 171,421.44 |
| 21 | **Libya** | 1,045.00 | 3,737.00 |
| 21 | **Libya** | 1,045.00 | 3,737.00 |
| 22 | **Iran** | 26,593.64 | 166,732.35 |
| 23 | **Marekani** | 74,186.00 | 453,618.00 |
| **Jumla** | | **1,301,888.12** | **6,770,950.22** |

**Chanzo:** Bodi ya Korosho

**USAFIRISHWAJI WA KOROSHO KARANGA KUTOKA TANZANIA KWENDA NCHI MBALIMBALI KUANZIA SEPTEMBA 2022 HADI JULAI 2023.**

## Jedwali Na. 6c: Uzalishaji na Usafirishaji wa Korosho Ghafi Kuanzia Msimu wa 2013/2014 hadi 2022/2023.

| UZALISHAJI NA USAFIRISHAJI WA KOROSHO GHAFI KUANZIA MSIMU WA 2013/2014 HADI 2022/2023. | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MWAKA | UZALISHAJI (TANI) | USAFIRISHAJI (TANI) | ASILIMIA ZA USAFIRISHAJI | MABADILIKO(%) |
| 2013/2014 | 130,123.778 | 117,012.708 | 89.92 | ► 0.0% |
| 2014/2015 | 198,114.034 | 180,817.844 | 91.27 | ▲ 1.5% |
| 2015/2016 | 155,244.645 | 153,087.745 | 98.61 | ▲ 8.0% |
| 2016/2017 | 265,146.980 | 254,912.380 | 96.14 | ▼ 2.5% |
| 2017/2018 | 313,826.386 | 292,338.802 | 93.15 | ▼ 3.1% |
| 2018/2019 | 225,304.977 | 209,517.522 | 92.99 | ▼ 0.2% |
| 2019/2020 | 232,681.798 | 215,920.558 | 92.80 | ▼ 0.2% |
| 2020/2021 | 210,786.804 | 204,158.346 | 96.86 | ▲ 4.4% |
| 2021/2022 | 240,158.752 | 225,222.808 | 93.78 | ▼ 3.2% |
| 2022/2023 | 189,113.799 | 169,111.648 | 89.42 | ▼ 4.6% |
| **Jumla** | **2,160,501.953** | **2,022,100.361** | **93.59** | ▼ |




**Chanzo:** Bodi ya Korosho

**NB:** Ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji na usafirishaji nje ya nchi kwa msimu wa 2023/2024 unaendelea.

**ALAMA ZINAONESHA MWENENDO WA MABADILIKO YA USAFIRISHAJI KATI YA MWAKA NA MWAKA**

**Usafirishaji umeshuka.** ▲ (bluu)

**Hakuna mabadiliko ya usafirishaji.** ▲ (nyekundu)

**Usafirishaji umeongezeka.** ▲ (kijani)

## JEDWALI NA. 6D: KOROSHO ZILIZOUZWA KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI.

| JUMLA YA KIASI KILICHOUZWA NA THAMANI HADI JULAI, 2023 | | |
|---|---|---|
| **KIPINDI CHA** | **KIASI KILICHOUZWA (KG)** | **THAMANI (TZS)** |
| Mwezi Julai | - | - |
| Jumlishi Oktoba-Juni | 176,749,451 | 328,362,003,965 |
| **JUMLA** | **176,749,451** | **328,362,003,965** |

## JEDWALI NA. 6E: MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MINADA

| MUHTASARI BEI ZA KOROSHO GHAFI KATIKA MNADA | | | |
|---|---|---|---|
| **MWEZI ULIOPITA (JUNI, 2023)** | | **MWEZI WA SASA (JULAI, 2023)** | |
| **MWENENDO WA BEI** | **Mwezi** | **Daraja la Kawaida** | |
| | | **Bei ya Juu** | **Bei ya Chini** |
| | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | Bei ya Mwezi Juni | 1,420 | 1,420 |
| | Mabadiliko (%) | | |

**UFUNGUO** “NA”= Haipo

| BEI YA MAUZO KOROSHO GHAFI YA MKOA (JULAI, 2023) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MKOA | CHAMA KIKUU | MWEZI | DARAJA LA KAWAIDA | |
| | | | BEI YA JUU | BEI YA CHINI |
| MTWARA | MAMCU | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,705 | 1,680 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| | MAMCU | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,605 | 1,604 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| LINDI | RUNALI | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,770 | 1,600 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| | LINDI MWAMBAO | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,726 | 1,726 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| PWANI | CORECU | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,520 | 1,520 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| RUVUMA | TAMCU | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,605 | 1,605 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| MOROGORO | MOFACU | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,721 | 1,721 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| TANGA | TACACU | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,420 | 1,420 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| DODOMA | DOMASIKA | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,720 | 1,720 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |
| SINGIDA | CEAMCU | Bei ya Mwezi Julai | NA | NA |
| | | Bei ya Mwezi Juni | 1,805 | 1,805 |
| | | **Mabadiliko (%)** | | |

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania



# KOROSHO MARATHON

Maandalizi ya Mbio za Korosho
Msimu Wa Pili **2023**

# MBIO ZA KOROSHO

Bodi ya Korosho inaendelea na maandalizi ya mbio za korosho **(Korosho Marathon)** kwa msimu wa pili. Uzinduzi wa usajili wa washiriki ulifunguliwa rasmi Julai Mosi, 2023 viwanja vya mashujaa Mtwara mjini. Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika tarehe 2 Septemba, 2023 Mtwara mjini na malengo ya mbio hizo ni kuhamasisha ulaji wa korosho karanga na matumizi ya bidhaa zinazotokana na korosho nchini.



**Msimu Wa Pili 2023**

#KoroshoMarathon
#MtwaraYetu

# ZAWADI KWA WASHINDI WA KOROSHO MARATHON MSIMU PILI WANAUME NA WANAWAKE.

| Mshindi | Zawadi ya Mshindi 21.1km | Zawadi ya Mshindi 10km |
|---|---|---|
| MSHINDI WA KWANZA | 4,000,000 | 2,500,000 |
| MSHINDI WA PILI | 3,000,000 | 2,000,000 |
| MSHINDI WA TATU | 2,000,000 | 1,000,000 |
| MSHINDI WA NNE | 1,000,000 | 700,000 |
| MSHINDI WA TANO | 900,000 | 500,000 |
| MSHINDI WA SITA | 800,000 | 400,000 |
| MSHINDI WA SABA | 700,000 | 300,000 |
| MSHINDI WA NANE | 600,000 | 200,000 |
| MSHINDI WA TISA | 500,000 | 100,000 |
| MSHINDI WA KUMI | 400,000 | 50,000 |



# TICC | Tanzania International Cashew Conference 2023

11-13 Oktoba, **2023**

# 6.0 MKUTANO WA KIMATAIFA WA KOROSHO 2023.




Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi zinazoongoza kwa uzalishaji korosho duniani, huku ikishika nafasi ya pili katika bara la Afrika na nafasi ya sita duniani kwa mujibu wataarifa za African Cashew Alliance (2021). Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea na maandalizi ya mkutano wa kimataifa wa korosho nchini utakaoitwa **"Tanzania International Cashew Conference-TICC"** utakaofanyika kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2023 hadi 13 Oktoba, 2023, katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere.

TICC

TANZANIA INTERNATIONAL CASHEW CONFERENCE 2023.

Lengo la mkutano huo ni kuhamasisha maendeleo ya zao la korosho kwa kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika zao la korosho. Kupitia mkutano huo, inatarajiwa ushiriki wa wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi katika Nyanja za utafiti, utengenezaji mashine za usindikaji, viwanda vya ubanguaji na uwekezaji. Mkutano huo utaenda sambamba na maonyesho ya bidhaa zitokanazo na zao la korosho na teknolojia mbalimbali zinazotumika katika usindikaji wa bidhaa za korosho.

## 7.0 TAARIFA YA MAPOKEZI NA UGAWAJI PEMBEJEO ZA KOROSHO KWA MSIMU WA MWAKA 2023/2024

Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea na upokeaji na ugawaji wa pembejeo za zao la korosho kwa ajili ya msimu wa 2023/2024. Hadi kufikia tarehe 28 Julai tayari jumla yalita 1,934,325 za viuatilifu vya maji, Sulphur ya unga tani 28,946.975 mabomba 5,000 na magunia 396,900 zimepokelewa katika ghala za pembejeo kitaifa zilizopo katika mikoa ya Mtwara na Lindi na Pwani. Ugawaji wa pembejeo unaendelea ambapo hadi kufikia tarehe 28 Julai jumla ya tani 19,800 za Sulphur na lita 1,560,326 za viuatilifu vya maji vimegaiwa kwa mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma.





**Bodi ya Korosho Tanzania** imeanzisha ushirikiano na Jukwaa la Korosho Africa lijulikanalo kwa jina la **African Cashew Alliance (ACA)** katika kuratibu Mkutano wa Kimataifa wa Korosho Tanzania **(TICC)** ili kubadilishana taarifa na uzoefu wa namna bora ya uendeshaji wa mikutano na majukwaa ya Korosho kitaifa na Kimataifa.

# USHIRIKIANO



**USHIRIKIANO HUU, UNALENGA KUPANUA WIGO WA FURSA ZILIZOPO KWENYE TASNIA YA KOROSHO NCHINI TANZANIA NA KWENYE SOKO LA KIMATAIFA LA KOROSHO.**

## LIMETOLEWA NA
## BODI YA KOROSHO TANZANIA

Ni Taasisi Iliyo anzishwa kwa Sheria
Na 18 ya Mwaka 2009.


**MTWARA MAKAO MAKUU**

www.cashew.go.tz


**#Ajenda10/30**